
whiteness of snow, *kusema thuluji ni nyeupe.*

Predicate, n. (in grammar) [*neno lenyi habari ya kitu fullani*].

Predict, v. *toa habari mbele, tabiri, bashiri, agua.*

Prediction, n. *ubashiri, uaguzi.*

Predictive, a. *-a kubashiri, -a kuagua.*

Predilection, n. *kupenda sana, upendeleo, shauko.*

Predispose, v. *vuta kwanza, lekeza, kabilisha, ongoza.*

Predisposition, n. *kulekea, maelekeo.*

Predominance, n. *kuwa na nguvu, kuzidi, kushinda.*

Predominant, a. *-enyi kuzidi, -kubwa, -ingi, -enyi nguvu.*

Predominate, v. *pita, -wa na nguvu, -wa -ingi, zidi, shinda.*

Pre-eminence, n. *kutangulia, kuwa na sifa* [*fahari*] *zayidi, cheo kikubwa.*

Pre-eminent, a. *-enyi* **Pre-eminence,** *-a kuzidi, -a kupita.*

Pre-emption, n. [*kununua mbele ao kwanza*].

Pre-engage, v. *shughulisha kwanza, shurutisha mbele, ajirisha mbele.*

Pre-establish, v. *thubutisha mbele.*

Pre-exist, v. *-wa mbele* [*kwanza, awali*].

Pre-existence, n. *kuwa mbele,* &c.

Pre-existent, a. *-enyi kuwa mbele,* &c.

Preface, n. [*maneno ya kwanza ao ya mbele kitabuni, matangulizi, dibaji*].

Prefatory, a. *-a* **Preface.**

Prefect, n. *liwali* [*ma-*], *wali* [*ma-*].

Prefer, v. *taka zayidi, chagua mbele.*

Preferable, a. *afathali, zayidi, heri, -ema sayidi, bora.*

Preference, n. *upendeleo, kuchagua mbele, ihtiari, kutangulia, kutangulisa.*

Preferment, n. *kuzidishiwa cheo, kupata kasi bora, ubele, daraja.*

Prefigure, v. *onya mbele kwa mfano.*

Prefix, n. (in grammar) [*sehemu ya neno yenyi kutiwa mwanzoni, ndio mbele ya* **Root**].

Prefix, v. *weka mbele, tia mbele.*

Pregnancy, n. *mimba, uzito.* During pregnancy, *kati ya mimba.*

Pregnant, a. *-enyi mimba, zito*; (important) *-kubwa, -a maana, -a nguvu.* Pregnant with, *-enyi, -a kujaa, -a kuleta.* Be pregnant, *-wa na mimba, hamili.* This is a very pregnant word, *neno hili lachukua maana nyingi* [*mambo kathawakatha*].

Prehensile, a. *-enyi nguvu ya kukamata, -a kukamatia; -fahamifu.*

Prehistoric, a. *-a zamani za kale sana* [*zisizo na habari ya hakika*].

Prejudge, Prejudicate, v. [*kata maneno mbele ya kusikia vema*], *hukumu kwa haraka, wa upesi mno.*

Prejudice, n. [*kuchukia ao kupendelea isivyo akili, kuonea mabaya ao mema pasipo haki*]; (injury) *hasara, thulumu, kuthuru.*

—— v. *chukiza* [*pendeleza*] *kwa vibaya*; (damage) *thuru, hasiri, punguza.*

Prejudicial, n. *-a kuthuru, -a kuzuia, -a kuhasiri, -a shari.*

Prelacy, n. *uaskofu, jamii ya maaskofu.*

Prelate, n. *askofu* [*ma-*].

Prelatic, Prelatical, a. *-a askofu, -a kiaskofu.*

Preliminary, a. *-a mwanzo, -a mbele, -a kufanya tayari.* Preliminary remarks, *matangulizi.*

Prelude, n. [*mwanzo wa kuimba, ao wa kupiga ngoma, maneno ya mwanzo, dibaji*].

Premature, a. *-a mbele ya wakati wake, -a haraka, -epesi.*

Prematurely, adv. *upesi, mbele ya wakati.*

Premeditate, v. *waza mbele, asimu mbele.*

Premier, n. *wasiri* [*ma-*] *mkuu.*

—— a. *-a kwanza, -kuu.*

Premise, n. [*asili ao chanzo cha maneno katika kujadiliana, hoja*].

—— v. *sema kwanza, patana mbele* [*kwa neno fullani*].

Premises, n. [*nyumba na pa kuizunguka, uwanja, kipenu, bustani*, &c.] *kiwanja, nyumba*; (in argument, premisses) *matangulizi, mategemeo, hoja.*

Premium, n. *malipo ya mbele*; (honorarium) *ada, zawadi*; (advance in price) *fayida.* Be at a premium, *zidi kuwa ya thamani, zidi bei, -wa shidda, ghalika.*

Premonish, v. *onya mbele, shauri, rudi.*

Premonition, n. *maonyo, shauri.*

Preoccupation, n. *kutwaa* [*kutwaliwa*] *mbele*; (being busy) *kushughulika.*

Preoccupy, v. *shika kwanza, kamata mbele*; (engage before) *shughulisha.*

Preordain, v. *amuru mbele, agiza mbele.*

Prepaid, a. *-liokwisha lipiwa kodi.*

—— p. t. *na* pf. t. *ya* **Prepay.**

Preparation, n. *kutengeneza mbele, fanya tayari, matengeneso, kuweka tayari, kuandaa*; (mixture) *changanyiko* [*ma-*], *dawa.* Make preparations for, *andalia.*

Preparative, Preparatory, a. *-a mbele, -a kwanza, -a kuwa tayari, -a kuandaa, -a mbele.*

Prepare, v. *fanya* [*weka*] *tayari, andaa, zatiti, tayari*, (neut.) *jiweka tayari, jiandaa*; (make) *fanyiza*; (cook) *pika*; (raw material) *chambua.* Prepare for, *andalia.*

Prepay, v. (p. t. *na* pf. t. **Prepaid**) *lipa mbele, lipia kodi mbele.*

Prepense, a. *-liokusudiwa mbele.*

Preponderance, n. *kuwa* **Preponderant.**

Preponderant, a. *-a kuzidi, -kubwa, -ingi.*

Preponderate, v. *zidi, -wa na nguvu* [*wingi*] *zayidi.*

Preposition, n. (in grammar) [*neno la kutiwa mbele ya* **Noun**, *lisilotengeka nalo*].

Prepossess, v. = **Preoccupy**; (attract) *pasha shauko, tamanisha.*

Prepossessing, a. *-zuri, -a kuvuta, -a kutamanisha.*

Prepossession, n. = **Prejudice**; (favourable) *shauko, upendeleo.*

Preposterous, a. *si desturi, si taratibu, -a kigeni, -baya, -siofaa.* Preposterous assertions, *maneno makuu, upuzi mtupu.*

Prerequisite, n. *kanuni, sharti.* It is a prerequisite, *sharti hii kwanza.*

Prerogative, n. [*haki ao mamlaka ao milki ya mtu mmoja peke yake, ao ya watu wenyi daraja ao kazi moja*], *haki ya desturi, haki ya asili, sharti, ubele.* Be the prerogative of, *husu.*

Presage, v. *onya mbele, agua, bashiri mambo yatakayokuja.*

—— n. *dalili, onyo* [*la mambo yatakayokuja*].

Presbyter, n. *mzee wa kanisa, kasisi, padre* [*ma-*].

Presbyterian, a. [*-enyi kusema, 'makasisi watosha, pasiwe maaskofu, katika kanisa'*].

Presbytery, n. [*jamii ya wazee wa kanisa, jamii ya makasisi*].

Prescience, n. *kuona mbele* [*mambo yatakayokuwa*], *busara.*

Prescient, a. *-enyi* **Prescience.**

Prescribe, v. *amuru, agiza.*

Prescription, n. *amri ya daktari, dawa iliyoamriwa*; (if forbidding something) *mwiko* [*mi-*]; (usage) *desturi, kuzoea, matumizi ya zamani.*

Prescriptive, a. *-a desturi tangu zamani.*

Presence, n. *kuwapo, kuwa karibu, eneo, pao mbele, machoni*; (appearance) *sura, umbo.* In the presence of, *mbele ya, machoni pa, panapo.* Presence of mind, *uelekevu wa akili, akili, busara, macho.*

Presence-chamber, n. *baraza, sebule.*

Present, n. (*Tax.* **Gift**) *zawadi, bakshishi, tuzo, tunu, majazo, kipaji, karama, wapo*; (customary) *ada, ufito, kilemba*; (reward) *tuzo*; (gratuity) *bakshishi*; (from God) *thawabu, upaji, baraka*; (of congratulation) *pukuso* [*ma-*]; (time) *wakati uliopo, wakati wa sasa, siku*

kizi. Give away as a present, Make a present of, *toa burre, tunukia.*

Present, a. (place) *karibu, mbele, -liopo, kapa, pale*; (time) *-a sasa, siku hizi, -a wakati huu*; (at hand) *-a marra moja, tayari*. Be present, *-wapo*. He is present, *yupo hapa, yupo*. At present, For the present, *sasa, wakati huu.*

—— v. (give) *-pa, toa, karimia, tunukia, jalia*; (put forward) *toa mbele, weka mbele* [*wazi*], *onyesha*; (arms) *lekeza, shika mbele*. Present by way of congratulation, *pukusa.*

Presentable, a. *-a kupalika, -a kupeka*; (pleasing) *-a kupendeza, -zuri, -a kufaa.*

Presentation, Presentment, n. *kupa, kutoa, kuweka mbele.*

Presentiment, n. *moyo wa kuona mbele*; (of fear) *hofu*; (of hope) *taraja.*

Presently, adv. *kalafu, baadaye, bado kidogo.*

Presentment, n. *kupa, kutoa,* &c. (*Tas.* **Present,** v.); (appearance) *sura, mfano.*

Preservation, n. *kulinda, kuhifathi, wokovu, kupona, uzima, salama*

Preservative, a. *-a kulinda, -a kuponya.*

Preserve, v. *linda, hifathi, okoa, ponya*; (keep) *weka, shika*; (season) *kolea, unga,* [*tia sukali chumvi,* &c., *kitu kisiose*].

—— n. *maandasi ya matunda*; (for game, &c.) [*mahali pa kuwekea na kulindia salama nyama, ndege, samaki, vyovyote vya kufuga na kuwinda*].

Preside, v. *-wa mkuu, tawala.*

Presidency, n. [*kazi, nyumba, wilaya, ya* **President**].

President, n. *mkuu, msimamizi.*

Presidential, a. *-a* **President.**

Presignify, v. *onya mbele, bashiri.*

Press, v. *songa, songanisha, sukuma, shindika, shindilia, kaza*; (with hand, fingers) *kamua, finya, bonyesha*; (as in vice) *bana*; (urge) *omba sana, sihi, bidisha, shurutisha, harakisha, sukumiza, nyenya*; (impend) *-wa karibu, lemea, taka haraka*; (force) *tumisha kwa nguvu*; (with argument) *hoji, shurutisha, chagiza.*

Press, n. *shinikizo, kinu*; (throng) *masongano, ghasiya ya watu, watu wakisongana*; (hurry) *haraka, shidda, taabu*; (machine) *mtambo*; (for printing) [*mtambo wa kupiga chapa vitabu*]; (printing) [*kazi ya kupiga chapa na kutoa vitabu*]; (news-writers) [*jamii ya watu wenyi kazi ya kutangaza habari ya mambo ya killa siku, watengenezaji wa* **Newspapers**].

Press-gang, n. [*asikari wenyi kukamatia watu kwa amri na kazi ya serkali*].

Pressing, n. *kusonga, kuomba,* &c. (*Tas.* **Press,** v.).

—— a. *-a haraka, -a kulemea, -a nguvu, -a shuruti.*

Pressure, n. *shinikizo, msongo, uzito, mshurutisho*; (trouble) *shidda, taabu, shughuli nyingi.* Use moral pressure, *bidisha, shurutisha, vuta.* He did it under pressure, *alifanya kwa nguvu.*

Prestige, n. *sifa* [*kwa ajili ya matendo ya zamani, ya mambo yaliyopita*], *heshima, fahari, jina.*

Presumable, a. *-lio yamkini, -lio wezekana.*

Presume, v. (dare) *thubutu, fanya pasipo ruhusa* [*pasipo haki*]; (suppose) *thania mbele, thania pasipo kujua, ona, waza.*

Presuming, a. *-fithuli, -juvi, -a kiburi.*

Presumption, n. *kiburi, ufithuli, majivuno*; (likelihood) *sababu, hoja*; (probability) [*kitu kilicho yamkini ao cha kuwezekana, kisicho hakika*].

Presumptive, a. *-a kutazamiwa, -a kusadikiwa, -a kutarajiwa.*

Presumptuous, a. *-a kiburi, -a kujasiri mno, -kuu.*

Presuppose, v. [*thania mbele ya kujua, kubali pasipo mathubutu*];

(imply) *-wa kwa sababu ya* [*kitu fullani kilichotangulia*].

Presupposition, n. [*jambo ao neno lisilothubutika, lathaniwa tu kuwa ndivyo, la ruhusa si la hakika*]; (reason) *sababu, mwanzo, asili.*

Pretence, n. (falsehood) *uwongo, hila, ujanja*; (pretext) *maneno, uthuru, sababu, kisingizo.*

Pretend, v. *jifanya, sema kwa uwongo, fanya hila, jisingizia.* Pretend to, *taka, tamani, jidaia.*

Pretender, n. *mdai* [*wa-*], *mwenyi kudai.*

Pretension, n. *kutaka makuu, kujidai kiburi*; (pretext) *maneno ya hila, uthuru, kisingizo*; (fiction) *uwongo*; (claim) *madai.*

Pretentious, a. *-a fahari, -a kujivuna, -kuu.*

Preterite, n. = **Past Tense.**

Pretermission, n. *kupitia*, &c.

Pretermit, v. *acha, ruka, pitia, pisha.*

Preternatural, a. [*-sio kawaida ya vitu vyote, -sio desturi*], *mwujiza, -geni, -a ajabu, -a kutisha.*

Pretext, n. *uthuru, sababu, maneno, hoja.*

Prettily, adv. *vizuri.*

Prettiness, n. *sura nzuri, uzuri.*

Pretty, a. *-zuri* [*kwa kutazama*], *nakawa, -enyi sura nzuri, -a kupendeza.*

—— adv. *kadiri, sana kidogo.* Pretty hot, *moto mwingi kidogo, jua kali.* I am pretty well, *sijambo kidogo.*

Prevail, v. (predominate) *shinda, weza, -wa na ngwvu*; (spread) *enea, -wa -ingi, -wa pote, -wa -kubwa, -wa siku zote.* Prevail upon, *shawishi, vuta, shinda, shurutisha.*

Prevailing, a. *-a kushinda*, &c. The prevailing wind, *upepo uliopo* [*ulio mwingi, ulio wa siku zote*]. The prevailing sentiment, *watu wengi waonavyo.* The prevailing fashions, *mtindo wa sasa.*

Prevalence, n. *maeneo*; (predominance) *kushinda*, &c., *kuchaga.*

Prevalent, a. *-a kuenea, -wa pote* [*-ingi, -kubwa, wakati wote*]. Fever is prevalent, *homa imechaga.*

Prevaricate, v. *sema uwongo, toa maneno ya ujanja, badilisha maneno.*

Prevarication, n. *uwongo, ujanja.*

Prevaricator, n. *mwongo, mjanja, kaoleni, mtu wa maneno mawili.*

Prevent, v. *zuia, pinga, komesha.*

Prevention, n. *kuzuia, zuio.*

Preventive, a. *-a kuzuia, -a kulinda, -a hathari.*

Previous, a. *-a kwanza, -a mbele, -a zamani.* Previous to, *mbele ya.*

Prey, n. *mawindo, mateka, nyara.* Beast of prey, *nyama mbuaji, nyama mkali.* Be the prey of, *shikwa na, patika na, shindwa na.*

—— v. Prey on, *-la, teka, haribu*; (harass) *lemea, huzunisha.*

Price, n. *kima, thamani, kiasi, bei*; (reward) *ijara, thawabu*; (return) *fayida, uchumi.* At the price of, *kwa ajili ya, kwa kutoa.* At any price, *kwa vyovyote.*

—— v. *tia kima, kadirisha.*

Priceless, a. *-a thamani nyingi, bora sana, -sionunulika kwa fetha.*

Prick, v. *choma, washa.* Prick the ear, *tega* [*simika*] *sikio.*

Prickle, n. *mwiba* [*mi-*].

Prickly, a. *-enyi miiba.* Prickly heat, *vipele vya harara.* Prickly pear, [*gugu lenyi maua na miiba mingi sana*].

Pride, n. *kiburi, majivuno*; (display) *fahari, makuu*; (subject of boast) [*kitu cha kujivunia, kitu cha kusifiwa sana*] *tunu, moyo, kipenzi*; (best sort) *kipeo.* Pride of youth, *kujijetea ujana.*

—— v. Pride oneself on, *jetea, jikinaisha kwa, jivunia, jigamba kwa.*

Priest, n. (heathen) *kahini* [*ma-*]; (Jewish) *kohani*; (Christian) *kasisi* [*ma-*], *padre, padiri* [*ma-*].

Priestcraft, n. [*ujanja wa makahini ao makasisi*].

Priesthood, n. *ukohani, ukasisi*, &c.

Priestly, a. *-a* **Priest.**

Priestridden, a. [*-a kuonewa na* **Priest**].
Prig, n. *ajivunaye kwa elimu, mjuvi.* Be a prig, Be priggish, *jijuvisha.*
Priggish, a. *-a* **Prig.**
Prim, a. *taratibu, -zuri, kiasi.* She is prim, *hataki upuzi, yu baridi.*
Primacy, n. [*kazi na heshima ya askofu mkuu*].
Prima-donna, n. *mwimbaji mkuu* [*wa kike*].
Primal, a. *-a kwanza.*
Primary, a. *-a asili, -a kwanza*; (important) *-kubwa, -a maana, -a nguvu:*
Primate, n. *askofu mkuu.*
Prime, n. *mwanzo, uzuri, usitawi, uzima, ukamilifu, upeo*; (morning prayers) *sala ya alfajiri.*
—— a. *-a kwanza, -zuri sana, bora.*
—— v. *tia baruti* [*kifani mwa bunduki*]; (teach) *somesha mafundisho ya kwanza, erevusha, julisha mambo.*
Prime-minister, n. *waziri* [*ma-*] *mkuu.*
Primer, n. *masomo ya kwanza, kitabu cha kwanza chuoni, mlango.*
Primeval, a. *-a zamani za kwanza, -a kale.*
Priming, n. *baruti ya kifani*; (of engine) [*maji yakichanganyika na mvuke ndani ya* **Steam-engine**].
Primitive, a. *-a zamani za kwanza, -a kikale.*
Primness, n. *uzuri, utaratibu*; (affectedness) *kaya, kiburi, baridi.*
Primogeniture, n. *kuzaliwa wa kwanza, kurithi mtoto aliyezaliwa kwanza.*
Primordial, a. *-a kwanza.*
Primrose, n. [*ua dogo la kondeni Ulaya, rangi ya manjano*].
Prince, n. *mfalme, seyidi, sultani*; (king's son) *bin sultani, mtoto mwanaume wa mfalme.*
Princedom, n. [*hali au heshima ya* **Prince**].
Princely, a. *-a* **Prince**, *-a kustahili* **Prince.**
Princess, n. *binti mfalme.*
Principal, n. *mkuu, msimamizi, bwana mkubwa*; (money) *ras il mali, akiba, asili ya mali.*
—— a. *kubwa, -kuu, -a maana, -a kwanza, -a nguvu.*
Principality, n. *inchi ya* **Prince.**
Principally, adv. *zaidi.*
Principle, n. *jambo la asili, neno la awali, chanzo* [*vy-*], *chimbuko* [*ma-*]; (rational rule) *mafundisho, mathehebu, kawaida*; (character) *tabia, moyo, nia*; (good character) *tabia nzuri, utu mwema*; (reason) *sababu.* High principle, *moyo mzuri, tabia nzuri.* He acts on principle, *ashika kawaida, afuasa mafundisho, hatendi ovyo, hana haraka.* These are his principles, *haya ndiyo mawazo* [*mashauri, mapenzi*] *yake.*
Print, v. *piga chapa, toa kitabu*; (mark) *tia kama alama*; (impress) *ingiza moyoni, tia moyoni.*
—— n. (mark) *chapa*; (picture) *sanamu*; (calico) *nguo ya rangirangi*; (printed words) *maneno yaliyopigwa chapa*; (of foot) *uayo* [*ny-*]; (finger, hand, &c.) [*alama ya*] *kidole, mkono*, &c.
Printed, a. *-a chapa, -liopigwa chapa.*
Printer, n. *mpiga chapa* [*vitabu*, &c.].
Printing, a. *kupiga chapa* [*vitabu*, &c.].
Prior, n. [*mkuu wa nyumba ya* **Monks**].
—— a. *-a kwanza, -a mbele.*
Priority, n. *kuwa mbele, ukuu.*
Priory, n. *nyumba ya* **Prior.**
Prism, n. [*kioo cha kuonyesha rangi za nuru mbalimbali, cha kugeuzia nuru nyeupe iwe rangi nyingi mbalimbali*].
Prismatic, a. (colours) [*rangi za nuru zilizoonekana kwa* **Prism**], *-a rangi mbalimbali.*
Prison, n. *kifungo, gereza, minyororo.*
Prisoner, n. *mfungwa* [*wa-*].
Pristine, a. *-a zamani za kale.*
Privacy, n. *faragha, pasipo watu,*

kujitenga, mahali pa siri, upweke, siri, kuficha, maficho.

Private, a. *-a* **Privacy,** *-a mwenyewe peke yake*; (retired, secluded) *-a faragha, -a upweke*; (unemployed) *pasipo kazi, pasipo nguvu, peke yake*; (unofficial) *si wa serkali.* Private life, *nyumbani.* Private property, *mali ya mwenyewe, mali ya watu.* Private means, *utajiri, mali.* This is my private opinion, *naona mimi.* A private person, *mtu tu* [*si mkubwa, si wa serkali*]. Privates, *pa siri, mbeleni.* A private (soldier), *asikari.* Private prayer, *sala ya siri, sala ya mtu peke yake.* In private, *faraghani, peke yake, kwa siri.*

Privateer, n. [*merikebu yenyi ruhusa kufanya vita pekeyake*].

Privation, n. *upungufu, ukosefu, kutwaliwa*; (poverty, want) *ukwasefu, mahitaji, shidda, taabu.*

Privative, a. *-a kunyima, -a kutwalia, -a kukana.*

Privilege, n. (special) *haki, mapendeleo, ruhusa, fayida, heshima, uweso* [*wa mtu mmoja peke yake*); (general) *sharti.* Be the privilege of, *husu.*

Privily, adv. *kwa siri, kwa mficho.*

Privity, n. *siri, maarifa ya siri, kuwa shauri moja kwa siri.*

Privy, a. *-a mtu mmoja peke yake*; (secret) *-a siri*; (retired) *-a faragha.* Be privy to, *jua kwa siri, shariki siri.* Privy council, *baraza ya mfalme mwenyewe* [*mawaziri, madiwani, wasiri wake*]. Privy councillor, *mtu wa* Privy council. Privy purse, *mali ya mfalme.* Privy seal, *muhuri ya mfalme.*

—— n. [*kijumba chenyi choo*].

Prize, n. (spoil) *mateka*; (reward in competition) *tuzo, tuza, zawadi*; (precious thing) *tunu, kitu cha thamani, azizi, dafina.*

—— v. *penda sana, pendelea, tunza sana, thani kuwa ya thamani nyingi, chunuka.*

Prize-fighter, n. *mshindani wa konde.*

Prize-money, n. *fedha ya* **Prize,** *tuzo.*

Probability, n. *hali ya kuwa* **Probable.** In all probability, *naona haina buddi.*

Probable, a. [*-a kutasamiwa lakini si hakika, -a kutarijiwa, -a kukofiwa, -takaokuwa*], *yamkini.* It is probable, *labuda, naona* (*Tav.* **Probably**). The probable result will be, *mwisho naona ndio huu.*

Probably, adv. *labuda, huenda, nathani, zayidi, inshallah, haikosi.*

Probate, n. [*mathubutu ya wosia ao kurithi*].

Probation, n. *majaribu.*

Probational, a. *-a kujaribu* [*kujaribiwa*].

Probationer, n. [*mtu anayejaribiwa kama atafaa kwa kazi fullani*], *mwanafunzi* [*wa-*].

Probe, v. *gusa* [*kwa sindano*], *pima*; (examine) *hoji, chungulia, tazamia.*

Probity, n. *uaminifu, unyofu, adili, wema, moyo mweupe.*

Problem, n. *swali* [*ma-*], *ulizo* [*ma-*]; (difficult matter) *mashaka, fumbo, neno gumu*; (riddle) *kitendawili.*

Problematic, a. *-a shaka, si hakika, ajabu.*

Proboscis, n. *mdomo* [*mi-*]; (of elephant) *mkono* [*mi-*].

Procedure, n. (formal) *utaratibu, kawaida*; (action) *ginsi ya kutenda, kazi*; (progress) *maendeleo, mwenendo.*

Proceed, v. (advance) *endelea mbele, enda, shika njia*; (come out) *toka*; (act) *fanya tena* [*zayidi*]. He proceeded to say, *tena akasema.* Proceed against, *shtaki, dai, peleka sheriani.*

Proceeding, n. *jambo* [*mambo*], *tendo* [*ma-*]. Take proceedings, *kwenda sheriani* [*kwa kathi*].

Proceeds, n. *pato* [*ma-*], *fayida, uchumi.*

Process, n. (method) *njia, ginsi*; (series) *mafuatano ya mambo*;

(operation) *kutenda, kufanya, kufanyika, kazi yenyewe.* In process of time, *baada ya siku, hatima.* Legal process, *da'wa, mashtaka, hukumu.*

Procession, n. *mafuatano, mwendo wa taratibu, andamo* [*ma-*], *wqtu wakiandamana.*

Processional, a. *-a* **Procession.**

Proclaim, v. *tangaza, piga mbiu ya, eneza, toa wazi, bainisha.*

Proclamation, n. *mbiu, amri wazi, utangazo, kunena wazi, ishtihari.*

Proclivity, n. *maelekeo*; (aptitude) *uelekevu.* He has a proclivity to steal, *huyu apenda uizi, tabia yake kuiba.*

Procrastinate, v. *sema 'kesho, kesho,' weka, kawia, legea, chelewa.*

Procrastination, n. *usiri, kukawia.*

Procreate, v. *zaa.*

Procumbent, a. *-a kulala fulifuli.*

Procurable, a. *-a kupatikana.*

Procure, v. *pata, patia, fanya, fanyiza, tengeneza, -wa sababu ya.*

Procurer, n. *wakili* [*ma-*]; = **Pander.**

Prod, v. *choma, chokora, piga kikumbo.*

Prodigal, a. *-potefu wa mali, -ponda mali, -fujaji, -bathirifu.*

Prodigality, n. *upotefu wa mali, kutapanya mali, ufujaji, ubathirifu.*

Prodigious, a. *-kubwa -ingi mno ajabu, ajabu sana.*

Prodigy, n. *mwujiza* [*mi-*], *ajabu* [*ma-*], *kioja* [*vi-*].

Produce, v. *toa, zaa*; (make) *fanya, fanyiza*; (cause) *-wa sababu ya*; (lengthen) *ongeza urefu*; (compose) *buni, tunga.*

—— n. *zao* [*ma-*], *mavuno, matunda*; (profit) *mapato, fayida, chumo.*

Producer, n. *mfanyizaji, mtenda kazi.*

Producible, a. *-a kuweza letwa, -a fanyiziwa, -liopatikana.*

Product, n. = **Produce,** n.; (of art) *kazi* [*ya fundi*]; (in arithm.) *jumla* [*katika* **Multiplication**].

Production, n. *kutoa, kufanyiza*; (lengthening) *kuongeza urefu*; (product) *kazi, mazao.*

Productive, a. *-a kuzaa, -a kutoa, -enyi kutoa -ingi, -zazi, hodari kwa kutoa* [*kufanyiza, kuzaa*].

Proem, n. *mwanzo wa maneno, dibaji.*

Profanation, n. [*kuharibu ao kutwesa ao kutumia vibaya kitu kitakatifu*], *unajisi, ukufuru.*

Profane, v. *kufurisha, tia unajisi* [*kitu kitakatifu*], *tia uchafu, haribu kwa taka, tumia vibaya.*

—— a. *-najisi, -baya, -a kumchukiza Muungu.*

Profaneness, Profanity, n. *ukufuru, unajisi, ubaya* [*wa kumchukiza Muungu*].

Profess, v. (declare) *toa habari wazi ya, tangaza*; (own, acknowledge) *shuhudia, ungama, kiri*; (claim for oneself) *jifanya, jipa sifa ya, jisifu* [*jidai*] *kuwa na, jitaji fundi wa.*

Professed, a. *wazi, baini, -a kujulika.*

Profession, n. *kunena wazi, ungamo, ushuhuda*; (promise) *ahadi*; (occupation) *kazi, uchumi, shughuli*; (class) [*jamii ya watu wenyi kazi moja*], *ufundi.*

Professional, a. *-a fundi wa kazi, -a kazi ya fundi, -a mwalimu.*

Professor, n. *mwalimu* [*wa-*], *fundi* [*ma-*], *ajifanyaye fundi.*

Professorial, a. *-a* **Professor.**

Proffer, v. *toa, -pa, taka kutoa.*

Proficience, Proficiency, n. *ustadi, welekevu, kuwa hodari*; (progress) *maendeleo.*

Proficient, a. *hodari, -enyi maarifa, -stadi, -elekevu, bingwa.*

Profile, n. [*sura ya mtu ao kitu kwa upande, si kwa mbele yake*].

Profit, n. *fayida, uchumi, chumo, mapato, kufaliwa, mafaa.*

Profitable, a. *-a kufaa, -a kuleta fayida.*

Profitless, a. *-sioleta fayida, -a burre, -siofaa, -tupu.*

Profligacy, n. [*hali ao tabia ya* **Profligate**], *upotofu,* &c.

Profligate, a. *-potofu, -fisadi, -fasiki, -asherati, -zinifu.*

Profound, a. (deep) *-a kwenda chini sana*; (significant) *-a maana sana*; (clever) *-a akili nyingi*; (great, much) *-kubwa, -ingi*; (enigmatic) *-a siri, -a fumbo.*

Profoundly, adv. *sana, kwa ndani, kwa bidii, kwa akili.*

Profoundness, Profundity, n. *kwenda chini,* &c. (*Taz.* **Profound**).

Profuse, a. *-ingi sana, tele*; (liberal) *-karimu, -paji, -enyi kutoa tele.*

Profuseness, Profusion, n. *wingi, neema*; (liberality) *ukarimu, upaji.*

Progenitor, n. *mzazi* [*wa-*], *baba.*

Progeny, n. *mzao* [*wa-*], *mtoto* [*wa-*], *mwana* [*wa-*].

Prognathous, a. [*-enyi taya mbele*].

Prognosis, n. [*kusema mbele ugonjwa utakuwaje*].

Prognostic, n. *ishara* [*dalili, ya mambo yatakuwaje baadaye*], *onyo* [*ma-*].

Prognosticate, v. *tabiri, bashiri, onya mbele, agua.*

Prognostication, n. *kuonya mbele, maaguzi.*

Prognosticator, n. *mwenyi kuonya mbele, mwaguzi, mpiga bau* [*falaki*].

Programme, n. *habari wazi* [*ya jambo linalokusudiwa*], *hati ya kutangaza habari, utaratibu.*

Progress, n. *maendeleo, mwendo, kuendelea mbele, ubele*; (journey) [*safari ya mfalme ao mtu mkubwa*].

—— v. *endelea mbele, shika njia, fanikiwa.*

Progression, n. *kuendelea mbele.*

Progressive, a. *-a kuendelea mbele, -a moja kwa moja, -a kidogo kidogo.*

Progressively, adv. *kwa kuendelea, kidogo kidogo, moja kwa moja.*

Prohibit, v. *kataza, gombeza, zuia, piga rufuka, rufuku.*

Prohibition, n. *makatazo, amri ya kugombeza, rufuka.*

Prohibitive, Prohibitory, a. *-a kukataza,* &c. (*Taz.* **Prohibit**).

Project, n. *shauri* [*ma-*], *nia, kusudi* [*ma-*], *azimu, mradi.*

—— v. *tupa mbele,* (neut.) *tokeza, fanya mdomo*; (design) *azimu, kusudia, fanya shauri ya, toa*; (sketch) *andika sanamu ya.*

Projectile, a. *-a kutupa mbele, -a kurusha.*

—— n. *kitu kilichotupwa* [*lisasi ya bunduki, mshale,* &c.].

Projection, n. *kutupa*; (thing projecting) [*kitu kitokezacho, mdomo, nundu, ushi* (*ny-*)]; (design) *kufanya shauri*; (drawing) *sanamu.*

Projector, n. *mtoa shauri, mtu wa mashauri mengi.*

Prolate, a. *-liopanuka, -liotanuka.*

Prolegomena, n. [*mafafanusi ao maelezo ya mbele kitabuni*], *matangulizi.*

Proletariat, n. *watu wanyonge, maskini, watu.*

Prolific, a. *-a kuzaa sana, -zazi sana*; (active) *-a kufanya mengi.*

Prolix, a. *-a maneno mengi, -a kuchosha, baridi.*

Prolocutor, n. *mnenaji, mnenea, mkuu wa mkutano.*

Prologue, n. *maneno ya mbele, mwanzo wa maneno, matangulizi.*

Prolong, v. *ongeza urefu, zidisha, dumisha, fuliza.*

Prolongation, n. *kuzidisha urefu, urefu wa kuzidi, mazidio, nyongeza.*

Promenade, n. *matembezi, mahali pa kutembelea.*

—— v. *tembeatembea.*

Prominence, n. [*kitu kitokezacho, kama mdomo, pua, nundu*]; (renown) *kujulikana, mashuhuri, ukubwa, sifa.*

Prominent, a. *-a kutokeza, -a kujulikana* (*Taz.* **Prominence**). Be prominent, *nyanyuka, onekana.*

Prominently, adv. *wazi, thahiri, mbele ya wote.*

Promiscuous, a. *-liotangamana, -sio taratibu, vivi hivi, -a fujofujo, -a*

shelabela, -ovyo. Make a promiscuous collection of, *panganya.*

Promiscuously, adv. *kifujo, -ote pamoja, ovyo.*

Promise, n. *ahadi*; (good prospect) [*kitu kitiacho*] *tumaini, taraja, kitu cha kutumainiwa.* Keep a promise, *fikiliza ahadi.* Break a promise, *vunja ahadi.*

—— v. *ahidi, toa ahadi*; (give prospect of) *tia tumaini, lekea mema.*

Promising, a. *-a kutumainiwa, -a kutaka mema, -a tabia njema, -a kulekea mema.*

Promissory, a. *-a ahadi, -enyi ahadi.* Promissory note, *hawala.*

Promontory, n. *rasi.*

Promote, v. *anzisha, endeleza, fanyiza, sayidia, ongeza*; (raise in rank) *-pa daraja, ongeza cheo, fanya -kubwa.*

Promoter, n. *mfanyizaji, mwendeleza, mletaji, mwongozaji.*

Promotion, n. *kupata daraja* [*cheo*], *kuzidishiwa heshima*; (setting forward) *kuanzisha,* &c. (*Tas.* **Promote**).

Prompt, a. *-epesi, -tendaji, hodari, tayari.*

—— v. *ongoza, sukuma, -pa moyo, tia bidii*; (in reading, &c.) *somesha.*

Prompting, n. *maongozi, shauri.*

Promptness, Promptitude, n. *wepesi,* &c. (*Tas.* **Prompt,** a.).

Promulgate, v. *toa wasi, tangaza, hubiri, eneza, bainisha.*

Promulgation, n. *kutoa wasi,* &c.

Prone, a. *fulifuli, tumboni*; (prone to) *-a kutaka, -a kulekea, -a kuzoelea, -zoefu wa.*

Proneness, n. *kulekea, kupenda, kuzoea.*

Prong, n. *uma* [*ny-*], *kiuma, chembe.*

Pronominal, a. *-a* **Pronoun.**

Pronoun, n. (in grammar) [*neno litumikalo mahali pa* **Noun**].

Pronounce, v. *ta'mka*; (declare) *nena wasi, tangaza.*

Pronounced, a. *wazi, thabiti, sana.*

Pronouncing, a. (dictionary, &c.) [*-a kuonya ginsi ya kutam'ka*].

Pronunciation, n. *matam'ko, usemi.*

Proof, n. (evidence) *ushahidi, ushuhuda, mathubutu, neno la kuthubutisha, sababu, hakika*; (trial) *jaribu* [*ma-*]; (strong spirit) [*mvinyo wa nguvu sana*].

—— a. *hodari, thabiti, -sioshindika, imara*; (impenetrable) *-siopenyeka.* Put to the proof, *jaribia, hakikisha.*

Prop, n. *mhimili* [*mi-*], *nguzo, tegemeo* [*ma-*]; (of ship, &c.) *gadi* [*ma-*], *shiku.*

—— v. *tegemeza, gadimu, shikiza, letea msaada.*

Propaganda, n. *maenezi* [*ya dini, mathehebu, maarifa,* &c.].

Propagandism, n. *bidii ya kueneza* [*dini, mafundisho,* &c.].

Propagandist, n. *mtu wa* **Propagandism.**

Propagate, v. *zaa, zalisha*; (spread) *-eneza, tangaza.*

Propagation, n. *kuzaa, kuzaliana*; (spreading) *kueneza, maenezi.*

Propel, v. *sogeza mbele, sukumia mbele, endeza, jongeza.*

Propeller, n. (of ship) [*gurudumu ya kuendesa merikebu ya moshi, pepeo*].

Propensity, n. *maelekeo, tamani, shauko, kutaka.*

Proper, a. *-a* [*hiyo fullani*] *peke yake*: (right) *-a adabu, -ema, -zuri, wajibu*; (suitable) *-a kufaa, -a kustahili*; (in strict sense) *halisi.*

Property, n. *mali, milki*; (nature, quality) *asili, hali, tabia, nguvu.* A man of property, *tajiri* [*ma-*].

Prophecy, n. *uaguzi, ubashiri, unabii.*

Prophesy, v. *toa unabii*; (predict) *agua, bashiri, tabiri.*

Prophet, n. *nabii* [*ma-*], *mtume* [*mi-*]; (foreteller) *mwaguzi, mbashiri, mwonya mbele.*

Prophetic, a. *-a nabii, -a kubashiri.*

Propinquity, n. *kuwa karibu, kupakana, ujirani.*

Propitiate, v. *tulisa, rithisha, patanisha.*

Propitiation, n. *kutuliza, kurithisha, kitulizo, kipatanisho.*

Propitiatory, a. *-a kutuliza*, &c. (*Tas.* **Propitiate**).

Propitious, a. *-a ndege njema, -a neema, -a heri, -a kupendelea.*

Proportion, n. *kadiri, ukadiri, kuwiana, ulinganifu, uzuri.*

—— v. *fanya kadiri, linganisha.*

Proportional, a. *-a kadiri.*

Proportionate, a. *-a kadiri, -linganifu, -a kufaa.*

Proposal, Proposition, n. *neno, maneno, jambo, kisa, shauri, nia, kusudi*; (of marriage) *kuulizia ndoa, kupoza, mapozo.*

Propose, v. *toa, toa shauri, leta maneno*; (intend) *kusudia, azimu, taka*; (advise) *shauri, onya*; (ask in marriage) *ulizia ndoa, poza.*

Propound, v. *toa, leta, nena.*

Proprietary, a. [*-a mtu fullani peke yake*], *-a mwenyewe.*

Proprietor, n. *mwenyeji, mwenyewe* [*w-*], *bwana.*

Proprietorship, n. *kumiliki, wenyeji.*

Propriety, n. *adabu, utaratibu, uzuri*; (suitability) *ulinganifu.*

Propulsion, n. *kusukuma, kupeleka mbele, msukumo.*

Propulsive, a. *-a kusukuma.*

Prorogation, n. *kuweka*, &c. (*Tas.* **Prorogue**).

Prorogue, v. *katiza* [*maneno ya baraza kuu*], *ahirisha, weka.*

Prosaic, a. *-a* **Prose, Prosy.**

Proscribe, v. *gombeza, kataza, harimisha.*

Proscription, n. *makataazo, kuharimisha.*

Prose, n. [*usemi wa maongezi ao wa siku zote, kuliko usemi wa mashairi na utenzi*]; (dull discourse) [*maneno ya baridi ao kuchosha*]. In plain prose, *wasi wasi.*

—— v. *toa maneno baridi* [*ya kuchosha*].

Prosecute, v. *shtaki mbele ya kathi, dai, peleka korti* [*sheriani*]; (carry on) *fuliza, endeza, shika kasi ya, dumia.*

Prosecution, n. *kudai, da'wa, mstaka* [*mi-*], *shtaka* [*ma-*]; (carrying on) *fulizo, kuendeza, kudumia.*

Prosecutor, n. *mshtaki* [*wa-*], *mdai.*

Proselyte, n. *niwongofu* [*wa-*] *wa dini.*

Proselytism, n. [*bidii mno ya kufanya* **Proselytes**].

Proselytise, v. *fanya* **Proselytism.**

Prosody, n. [*kanuni za kutunga mashairi*].

Prospect, n. *kutazamia mbele, mambo ya mbele, mambo yajayo*; (view) *yaliyo mbele ya macho, sura ya ulimwengu*; (ground of hope) *sababu ya kutumaini, matumaini.* There is a prospect of war, *inakabili vita.*

—— v. *peleleza, chungulia.*

Prospective, a. *-a mbele, -a baadaye*; (looking forward) *-a kutazamia mbele.*

Prospectus, n. *daftari, muhtasari.*

Prosper, v. (neut.) *fanikiwa, fana, ongokewa, kunjuka, sitawi, -wa na heri*; (make prosper) *fanikisha, sitawisha.* God prosper you, *Allah bilkheri, Muungu akubariki, Mwenyezi Mngu akuweke.* My affairs have prospered, *mambo yamenifanikia.*

Prosperity, n. *mali, usitawi, uheri, neema, mbaraka, kufanikiwa.*

Prosperous, a. *-enyi* **Prosperity.**

Prostitute, n. *kahaba* [*ma-*].

—— v. *fanya kahaba*; (abuse) *aibisha, tumia vibaya* [*kwa aibu*].

Prostitution, n. *ukahaba*; (abuse) *matumizi mabaya* [*ya aibu*].

Prostrate, a. *fulifuli, chini, -liolala chini*; (overcome, exhausted) *-legevu, -chovu, -a kuzimia roho.*

—— v. *angusha chini*; (exhaust) *shinda kabisa, legeza nguvu ya.* Prostrate oneself before, *sujudu, sujudia.*

Prostration, n. *kusujudu*; (exhaustion) *ulegevu wa nguvu, kuvunjika nguvu.*

Prosy, a. *-a baridi, -a vivi hivi, -a kuchosha.* It is prosy (dull), *haina kiungo.*

Protean, a. *-a mageuzi mengi, -a kugeukageuka.*

Protect, v. *hifathi, tunza, linda, ponya, funika.*

Protection, n. *hamaya, tunza, ulinzi*; (something that protects) *kinga, ngao, kifuniko.*

Protectionist, n. [*asemaye, 'zuieni biashara ya wangineo, mpate kusitawisha yenu'*].

Protective, a. *-a kuhifathi.*

Protector, n. *mhifathi, mlinzi, baba.*

Protectorate, n. *kamayat al serikali.* A British Protectorate, *inchi iliyo chini ya hamayat al Ingereza.*

Protectorial, a. *-a hamaya.*

Protégé, n. *mtoto* [*wa-*], *mtu* [*wa kulindwa*].

Protest, n. *ushuhuda, kushuhudia*; (objection) *makataso, udaku.*

—— v. *shuhudia, kataza, si kubali.*

Protestant, n. [*Mmasihiya asiyekubali mafundisho ya Kanisa la kirumi kwa mambo mangine ya dini*].

Protestantism, n. *hali ya* **Protestant.**

Protestation, n. *maneno ya kushuhudia* [*ya kukataza*].

Protocol, n. *kol, hati yenyi mapatano.*

Protomartyr, n. **Martyr** *wa kwanza.*

Prototype, n. *chanzo, cheo, kiolezo, namna ya asili* [*ya awali*].

Protract, v. *ongeza wakati wa, fuliza, zidisha, kawilisha.*

Protraction, a. *kukawilisha*, &c. (*Tas.* **Protract**).

Protrude, v. *toa nje, benua*; (neut.) *tokeza, toka nje, benuka, fanya mdomo* [*nundu*].

Protrusion, n. *kutoa, kutoka*, &c. (*Tas.* **Protrude**).

Protuberance, n. *kubenuka, kutokeza, uvimbi, nundu, mgongo.*

Proud, a. *-a kiburi, -a kujisifu, -a fahari.*

Provable, a. *-a kuweza kuthubutika*, &c.

Prove, v. *thubutisha, shuhudia, bainisha, hakikisha*; (turn out) *tokea, tekelea, onekana, bainika*; (try) *jaribu, jaribia, onja.*

Provender, n. *chakula* [*cha ng'ombe ao frasi*, &c., *majani, manyasi, malisha*].

Proverb, n. *methali, mfano wa maneno.*

Proverbial, a. *-a* **Proverb**; (generally known) *-a kujulika na wote, -a kuvumika kote.*

Provide, v. *toa, andaa, weka tayari, auni*; (provide for) *amuru mbele, tazamia mbele, -wa tayari kwa, wekea, akiba, andalia*; (support) *-wa riziki za, -wa akiba ya, -wa mali ya.*

Provided (that), conj. *kwa sharti ya, kama, iwapo.*

Providence, n. *Muungu, maongozi ya Muungu, amri ya Muungu, majaliwa*; (foresight) *busara, mawazo ya mbele, kutazamia mbele*; (thrift) *kuweka akiba, kukata gharama.*

Provident, a. *-enyi busara, -a kutazamia mbele, -a kuweka akiba.*

Providential, a. *-a* **Providence.**

Province, n. (function) *kazi, shughuli, sehemu*; (territory) *inchi, wilaya, jimbo* [*ma-*]; (class) *sehemu ya mambo, aina, jamii.* It is not my province, *simo, si juu yangu, si kazi yangu.* The provinces, *mashamba, miji midogo.*

Provincial, a. *-a mashamba, -a miji midogo*; (countrified) *-a kishensi, -a kishamba, -geni.*

Provincialism, n. *ushenzi, ugeni*; (in speech) *usemi wa kimashamba.*

Provision, n. *madaraka, kufanya tayari*; (clause, agreement) *sharti, maafikano.*

—— v. *wekea chakula.*

Provisional, a. *-a wakati kitambo, -a marra moja, si -a dayima.*

Provisions, n. *vyakula, makuli, riziki*; (for journey, &c.) *masarufi.*

Proviso, n. *sharti, maafikano.*

Provocation, n. *kukasirisha, jambo la kukasirisha.*

Provocative, Provocatory, a. *-a kukasirisha*; (causal) *-a kutoza, -a kufanya.*

Provoke, v. *kasirisha, ghairi, tia uchungu*; (cause) *fanya, -wa sababu ya, toza, leta.* Be provoked (take offence), *futuka.*

Provoking, a. *-a kukasirisha, -tiriri.*

Provost, n. *mkuu* [*wa-*]; (in Scotland) *liwali* [*ma-*].

Prow, n. *gubeti, omo*; (of small vessel) *kikomo.*

Prowess, n. *ushujaa, ujasiri, uthabiti, ugumu.*

Prowl, v. *zunguka-zunguka* [*kama simba usiku*].

Proximate, a. *-a karibu, -a pili yake, -a palepale.*

Proximity, n. *kuwa karibu, kupakana, ujirani.*

Proxy, n. *badala, wakili* [*ma-*].

Prude, n. *mwenyi* Prudery.

Prudence, n. *busara, fikara, hathari, utaratibu, akili.*

Prudery, n. *kuwa na haya mno, kujivunia haya, ubaridi.*

Prudish, a. *-enyi* Prudery.

Prune, n. [*tunda kama zambarau*]. —— v. *kata* [*punguzia*] *matawi, chenga, pogoa, fyeka.*

Prurience, n. *ng'oa, ufisadi, nyegi.*

Prurient, a. *-a* Prurience.

Pry, v. *chungulia, peleleza, dadisi.*

Psalm, n. *zaburi.*

Psalmist, n. *mtunga zaburi.*

Psalmody, n. *jamii ya zaburi, kuimba zaburi.*

Psalter, n. *kitabu cha Zaburi za Daudi.*

Psaltery, n. [*zeze la kiyahudi*].

Pseudonym, n. *jina la uwongo, jina la kubunika.*

Psychical, a. *-a roho ya binadamu.*

Psychological, a. *-a* Psychology.

Psychologist, n. *mwalimu wa* Psychology.

Psychology, n. [*elimu ya mambo ya roho ya binadamu*].

Puberty, n. *ubalihi, kuanza kuwa mtu mzima, kukomaa, upevu.*

Public, a. *-a wazi wazi, baini, -a watu wote*; (official) *-a serkali.* Public affairs, *mambo ya taifa, mambo ya serikali, mambo yapasayo wote, mambo makubwa.*

Publican, n. *mwenyi* Public-house; (tax-gatherer) *mtoza ushuru.*

Publication, n. *kubainisha, kueneza habari, kutoa wazi*; (book) *kitabu, kutoa kitabu.*

Public-house, n. *nyumba ya wageni* [*ya kukaribisha watu wo wote, pauzwapo mvinyo, pombe,* &c.].

Publicist, n. *mwalimu wa sheria.*

Publicity, n. *uwazi, ubayana, kujulikana.*

Public-spirited, a. *-karimu, -paji,* [*-a kukumbuka watu wote, -a kufathili watu kuliko nafsi yake*].

Publish, v. *bainisha, tangaza, toa wazi, eneza habari*; (of books, &c.) *toa, piga chapa, tembeza.*

Publisher, n. *mweneza habari*; (of books) *mtoa vitabu.*

Pucker, v. *kunja, finya.*

Pudding, n. *maandasi, pudini.*

Puddle, n. *kiziwa cha maji, kidimbwi* [*vi-*].

Puddling, n. [*kama kutia matiko*].

Puerile, a. *-tiriri, -a kitoto, -a kuchezacheza.*

Puerility, n. *utiriri, kuchezacheza.*

Puerperal, a. *-a uzazi.*

Puff, n. *kishindo* [*cha pumuzi ao cha pepo*]; (overpraise) *maneno ya kusifu mno*; (pastry) [*maandasi*]. —— v. *puliza kwa kishindo, toa* [*tia*] *pumuzi kwa kishindo*; (pant) *tweta, kokota roho*; (inflate) *jaza* [*vimbisha kwa*] *hewa*; (praise unduly) *sifu mno, tembeza, angaza*; (make swell) *furisha.*

Puffy, a. *-a kuvimba, -a kufura.*

Pugilism, n. *maarifa ya kupigana konde.*

Pugilist, n. *mpigana konde.*

Pugilistic, a. *-a kupigana konde.*

Pugnacious, a. *-gomvi, -a kutaka vita, -piganaji, -kali.*

Pugnacity, n. *kutaka vita, ushindani.*

Puissant, a. *-a enzi, -a nguvu kuu.*
Pull, n. *mvuto, nguvu ya kuvuta, uweso*; (carrying on) *mfulizo.*
—— v. *vuta, kokota*; (pluck) *chuma.* Pull down, *angusha, bomosha.* Pull up, *simamisha,* (neut.) *simama*; (root up) *ng'oa.* Pull through, *pona, okoka.* Pull a face, *kunja uso, finya uso.*
Pullet, n. *kuku mdogo, mtoto wa kuku, faranga* [*ma-*].
Pulley, n. *kapi* [*ma-*], *ayari.*
Pulmonary, a. *-a kifua, -a pafu* [*ma-*], *-a pumu.*
Pulp, n. [*kitu kilicho chororo, kama nyama ya tunda bivu, kama ubongo*].
Pulpit, n. *mimbara.*
Pulpy, a. *kama* **Pulp.**
Pulsate, v. *pigapiga, puma, tutuma.*
Pulsation, n. *kupigapiga, kupuma.*
Pulse, n. *kupigapiga moyo, pigo la mshipa wa damu*; (grain) *nafaka.* Feel the pulse, *kanda mshipa.*
Pulverize, v. [*fanya kama unga*] *ponda, tua, saga.*
Puma, n. [*nyama wa Amerika, kama simba*].
Pumice, n. [*jiwe jepesi, litokalo katika* **Volcano**].
Pummel, v. *na* n. = **Pommel.**
Pump, n. *bomba* [*ya kupandisha maji juu*].
—— v. *vuta kwa bomba*; (question) *hojihoji, dadisi.*
Pumpkin, n. (plant) *mboga* [*mi-*]; (fruit) *boga* [*ma-*].
Pun, n. [*neno la ubishi lenyi maana mbili*], *usumi.*
—— v. [*chezea maneno, sema maneno yenyi maana mbili kwa ubishi*].
Punch, n. [*mvinyo wa moto uliotiwa sukali, karafuu,* &c.]; (tool) [*chuma cha kuchomea ao kuzulia*]; (puppet) [*mtoto wa bandia, kinyago*].
—— v. *piga konde.*
Punctilio, n. *utaratibu halisi, adabu, ustahifu.*
Punctilious, a. *-enyi* **Punctilio.**
Punctual, a. *-enyi* **Punctuality,** *sawa sawa* [*wakati*], *barabara.* Be punctual, *kumbuka saa, si chelewa.*
Punctuality, n. *kushika wakati wake, kuja kwa wakati wake, sawa sawa, barabara, -siochelewa.* Punctuality is indispensable, *sharti killa kasi kwa saa yake barabba.*
Punctuate, v. *tia* **Punctuation.**
Punctuation, n. [*alama za kutenga maneno, na kuonya vikomo, kama hizi* (; , . ! :)].
Puncture, v. *choma* [*kwa sindano*].
—— n. *kitundu* [*vi-*].
Pungency, n. *uchungu, ukali.*
Pungent, a. *-chungu, -kali.*
Punish, v. *athibu, rudi, lipa, athibisha.*
Punishable, a. *-a kustahili athabu, -a kupasiwa hukumu, haramu.*
Punishment, n. *athabu, malipo, marudio.*
Punitive, a. *-a kuathibu, -a athabu.*
Punkah, n. *pepeo* [*ma-*] *kubwa, panka.*
Punster, n. *mfanya* **Pun.**
Punt, n. [*mashua ya mbau iliyo sawa chini, haina mkuku*].
—— v. *endesha* [*mashua*] *kwa pondo.*
Puny, a. *-dogo, thaifu sana, -liovia.*
Pup, n. *mtoto wa mbwa.*
—— v. *zaa* [*mbwa*].
Pupa, n. [*nyumba ao tundu la mdudu*] *mdudu* [*wa-*]; (of bee) *jana* [*ma-*].
Pupil, n. *mwanafunzi* [*wa-*]; (of eye) *mboni ya jicho, kiini cha jicho, mwana wa jicho.*
Puppet, n. *mtoto wa bandia.*
Puppy, n. = **Pup,** n.
Purblind, a. *nussu kipofu, macho thaifu.*
Purchase, v. *nunua, pata kwa fetha, pata.*
—— n. *kununua, ununuzi*; (thing bought) [*kitu kilichonunuliwa*], *nunuzi* [*ma-*]; (instrument) *chimbuko la nguvu, chombo, egemeo, msaada.*
Purchaser, n. *mnunuzi* [*wa-*].
Pure, a. *safi, -eupe, fasihi, -takatifu*; (unmixed) *-tupu, tu, peke yake, halisi.*
Purely, adv. *halisi, haswa, tu.*
Pureness, n. *kawa* **Pure.**

Purgative, n. *dawa la kuharisha* [*ka kufungua choo, la kuendesha choo*].

Purgatorial, a. *-a* **Purgatory.**

Purgatory, n. [*mahali pa ahera pa kutakasia thambi ndogo*].

Purge, v. *takasa, safisha*; (clear) *ondolea taka* [*hatiya*]; (evacuate) *harisha.*

Purification, n. *utakaso*; (ceremonially) *weuo, tohara.*

Purificatory, a. *-a kutakasa, -a kueua.*

Purify, v. *takasa, safisha, chuja*; (ceremonially) *eua*; (correct) *sahihisha.*

Purist, n. *fasihi* [*wa maneno, usemi, adabu,* &c.].

Puritan, n. [*watu walioshindana na Kanisa la Ingeresa zamani za* **Reformation**, *wakitafuta dini iliyo safi zayidi; mtu ajivunaye kuwa na dini safi*].

Puritanical, a. *-a* **Puritan.**

Puritanism, n. [*mathehebu ya* **Puritan**].

Purity, n. *utakatifu, kuwa safi, weupe*; (ceremonial) *tohara*; (correctness) *ufasihi, uhalisi, ubora.*

Purlieu, n. *kiunga* [*vi-*].

Purloin, v. *iba, nyang'anya.*

Purple, n. *wekundu* [*kama zambarau mbivu*]; (royal) *vasi la kifaume*; (sovereignty) *ufalme, ensi.*

Purport, n. *maana.*

Purpose, n. *kusudi* [*ma-*], *kasidi, nia, shauri, mradi.* Serve a purpose, *faa.* On purpose, With the purpose, *makusudi.* He coughed on purpose (purposely), *alijikohoza.* To the purpose, *-enyi njia, -a kufaa, -a maana.* To small purpose, *burre, isivyofaa.*

—— v. *kusudia, azimu, taka.*

Purposeless, a. *pasipo shauri, -a burre, -pumbafu, -batili.*

Purposely, adv. *makusudi.*

Purr, n. [*mvumi wa paka kwa furaha yake*].

—— v. *toa* **Purr.**

Purse, n. *kifuko* [*cha kutilia fetha*]; (money) *mali*; (treasury) *hasina.* Make up a purse, *changa fetha.*

Purse-proud, a. [*mjivunia mali*].

Purser, n. *karani wa fetha* [*katika manowari*].

Pursuance, n. In pursuance of, Pursuant to, *kwa kufuata, kwa.*

Pursue, v. (drive off) *fukuza*; (hunt) *saka, winda*; (follow) *fuata, kimbilia*; (attend to, carry on) *shika, dumia, fuliza*; (aim at) *taka, tafuta, tamani.*

Pursuer, n. *mfukuzi, mkimbizi.*

Pursuit, n. *kutafuta, kutaka*; (chase) *ufukuzo, ukimbizo*; (occupation) *kazi, nchezo* [*mi-*], *shughuli, mambo.*

Pursuivant, n. *mjumbe* [*wa-*], *mtangulizi* [*wa-*].

Pursy, a. *-fupi na -nene.*

Purulent, a. *-enyi usaha.*

Purvey, v. *patia chakula, nunulia chakula.*

Purveyor, n. *mtoa chakula.*

Purview, n. *eneo.*

Pus, n. *usaha.*

Push, v. *sukuma*; (accelerate) *himiza, endesha mbio*; (annoy) *sumbua, sukumiza*; (carry beyond bounds) *ongeza mno.* Be pushed for, *sidiwa, sumbukia, shidda kupata.* Push against, *kumba.* Push aside, *piga kikumbo, sukumia upande.* Push past, *pita karibu, ambaa.* Push off, *kumbisha.* Push on, *sogeza* [*jongeza*] *kwa nguvu*; (neut.) *enda haraka, kaza mwendo.* Push questions, *hojihoji.*

—— n. (in face) *mdukuo*; (with arm) *msukumo, kikumbo.*

Pushing, a. *-epesi, -pasi, hodari.*

Pusillanimous, a. *-oga, thaifu, -nyonge, -enyi roho chache.*

Puss, Pussy, n. [*jina la*] *paka.*

Pustule, n. *kipele* [*vi-*], *upele* [*pele*].

Put, v. (p. t. *na* pf. t. Put) *tia, weka.* Put across, over, in front of, *amba.* Put a stop to, *zuia, komesha.* Put about (ship), *pindua.* Be put about, *sumbuka, hangaika.* Put away, *wekea mbali, weka akiba, chelesa,*

ondosha; (a wife) *achana na, taliki.* Put back, *rudisha*, (neut.) *rudi.* Put between the legs, *fyata*; (of loin-cloth) *piga uwinda.* Put by, *ondoa*; (as store) *weka akiba.* Put down, *shusha, tua*; (lessen) *punguza*; (stop) *komesha, batilisha*; (write down) *andika*; (pay) *lipa.* Put forth (forward), *toa, nyosha*; (carry on) *endesha.* Put in, *ingiza*; (in purse, pocket, &c.) *futika*; (in the ground, ashes, leaves, &c.) *vumbika.* (come to shore) *-ja pwani.* Put in line, or in order, *panga, tunga, ratibisha.* Put in mind of, *kumbusha, fahamisha.* Put off, (clothes, &c.) *vua, ondoa*; (defer) *weka, akhirisha, cheleza*; (mislead) *danganya*; (leave shore) *toka pwani, tweka.* Put off on, *sukumizia, kumbishia.* Put on, (clothes, &c.) *vaa, valia, vika*; (arrow on string, knife in belt, spectacles on nose) *pachika*; (on lap, knees, shoulder) *pakata*; (assign) *amria*; (employ) *tumia*; (attribute) *sukumia*; (deceive) *punja, danganya*; (set to) *tia katika*; (on the fire) *teleka*; (on a spit) *tunga kijitini.* Put on guard, *tahathirisha, onya.* Put on trial, *peleka kukumuni*; (prove) *jaribu.* Put out, *toa, ondosha*; (extinguish) *zima, zimisha*; (dislocate) *stusha, tegua*; (extend) *nyosha, toa nje*; (perplex) *fathaisha*; (offend) *tia uchungu, kasirisha.* Be put out, *ona chuki, futuka.* Put over, *vukisha, abirisha*; (defer) *weka, akhirisha*; (make master of) *weka juu ya, fanya msimamizi wa.* Put through, *penyesha*; (carry out) *maliza, fikiliza.* Put to bed, *lasa kitandani, laza, tuesha.* Put to death, *fisha, ua.* Put to (door), *shindika.* Be put to, *sidiwa, sumbuka, fathaika.* Put to flight, *kimbiza.* Put to rights, *tengeneza.* Put to sea, *tweka.* Put to the sword, *chinja.* Put up, (lodge) *tua, panga*; (for sale) *usa, tembeza*; (set aside) *weka*; (pack) *funga*; (erect) *simamisha, jenga*; (game) *stusha* [*kimbisa*] *nyama.* Put up with, *vumilia, stahimili, subiri.* Put up to, *erevusha, onya, tia hathari ya, eleza, fundisha.* Put up for (apply for, ask work for), *andikia jina.*

Putative, a. *-liothaniwa lakini siyyo, -a uwongo.*

Putrefaction, n. *kioza, uvundo.*

Putrefy, v. *oza*; (act.) *ozesha.*

Putrid, a. *-enyi kuoza,* &c.

Putridity, n. *kioza, uvundo.*

Putty, n. (whiting) *chaki.*

Puzzle, v. *zuzua, tatanisha, fathaisha, shinda*; (use puzzling language) *fumba maneno.*

—— n. *matata, kitendawili, fumbo.*

Puzzling, a. *-a matata.*

Pygmy, n. *kibeti* [*vi-*], *mbilikimo* [*wa-*].

Pyramid, n. [*jengo la mawe, kama mapaa manne ya nyumba yaliyo sawa yote,* (Ar.) *haram*]; (pile) *chungu ya mawe, chungu.*

Pyramidal, a. *kama* **Pyramid.**

Pyre, n. *chungu ya kuni* [*ya kuzikia mtu*].

Pyrotechnic, a. *-a* **Pyrotechny.**

Pyrotechnics, Pyrotechny, n. [*kazi ya kufanya fataki, viberiti, mangine ya moto*].

Python, n. *chatu.*

Q

Qua, conj. *kwa kuwa.*

Quack, v. *lia* [*kama bata*]; (boast) *jivuna.*

—— n. *mlio* [*wa bata*]; (doctor) [*mtu ajifanyaye mganga asijue dawa*]; (impostor) *ayari, mwongo.*

Quackery, n. *dawa ya uwongo-uwongo, madanganya.*

Quadrangle, n. [*sanamu yenyi pande 'nne na pembe 'nne*; (court) *behewa kati ya nyumba, uwanja wenyi nyumba pande zote*].

Quadrangular, a. *kama* **Quadrangle.**

Quadrant, n. [*chombo cha kupimia kadiri ya kupanda jua ao nyota angani*].

Quadrilateral, a. *-enyi pande 'nne.*

Quadrille, n. [*ngoma ya Ulaya ya kucheza watu wanane, wawili-wawili*].

Quadroon, n. [*mtu nussu mweupe nussu mweusi*].

Quadrumanous, a. *-enyi mikono minne* [*kama nyani*].

Quadruped, n. [*nyama yenyi miguu minne*].

Quadruple, v. *sidisha marra 'nne.*

Quaff, v. *nywa kwa mashindo, gugumiza.*

Quagga, n. [*nyama kama punda milia*].

Quagmire, n. [*mahali penyi maji na matope yametanganana chini, ziwa baya la kulopeza watu*].

Quail, n. *tombo, tomboroko.*

—— v. *tetema kwa hofu, shindwa na hofu, jikunyata kwa hofu.*

Quaint, a. *-geni, ajabu, -a mtindo, -a peke yake, -a kuchesha.*

Quaintness, n. *kuwa* **Quaint.**

Quake, v. *tetemeka, tapatapa.*

—— n. *tetemo* [*ma-*].

Quaker, n. [*watu waliotengana na Kanisa kama* A. D. 1650, *wakajitaja 'Marafiki,' wakishika mathehebu zao wenyewe*].

Quakerism, n. [*mathehebu ya* **Quakers**].

Qualification, n. *sifa, tabia, hali, akili, ruhusa, uweso*; (change) *mageuzi, tofauti*; (disparagement) *upunguo, kupunguza sifa, kusahikisha.*

Qualify, v. *wezesha, stahilisha, tolea ruksa* [*haki, sifa, uwezo*]; (alter) *geuza, punguza*; (neut.) *pata kufaa* [*kuweza, kustahili*]. Be qualified, *faa, weza, stahili, -wa na akili, tumikana.* In qualified terms, *si sana, kidogo.*

Qualitative, a. *-a kuonya* **Quality.**

Quality, n. *tabia, ginsi, jisi, aina, sifa, cheo, cheo bora.* A person of quality, *mtu bora.*

Qualm, n. *kuchafuka tumbo*; (scruple) *uchungu, mashaka.*

Quantity, n. *kiasi, kadri, cheo, wingi, ukubwa.*

Quarantine, n. [*kuzuiwa mahali kwa sababu ya ugonjwa, watu wasiambukiswe*], *kifungo, kufungwa, kwarantini.*

Quarrel, n. *ugomvi, mateto, tofauti.*

Quarrelsome, a. *-gomvi.*

Quarrelsomeness, n. *ugomvi.*

Quarry, n. [*pa kuvunja ao kuchimba mawe*], *chimbo* [*ma-*]; (prey) *windo* [*ma-*].

Quarryman, n. *mvunja* [*wa-*] *mawe.*

Quart, n. [*kipimo cha Ingereza kama vibaba viwili, kisaga*].

Quartan, a. *-a killa siku ya 'nne.*

Quarter, n. *robo, sehemu ya 'nne*; (sparing life) *amani, kuachia* [*kuachiwa*] *maisha*; (of a town) *mtaa* [*mi-*]; (direction) *upande*; (weight) *ratli asharini na nane.* Three-quarters, *kassa robo.* Give quarter, *achia adui aishi, -pa amani, acha.* Quarter dollar (half rupee), *robo.* Quarter rupee (eighth of dollar), *themuni.* (*Tax.* **Quarters.**)

—— v. *kata vipande vinne*; (lodge) *kalisha, -pa kituo na chakula.*

